**TARGETER KCPE TRACKER**
**DARASA LA NANE - 2020**

**TRACKER 002**

# KISWAHILI

## SEHEMU YA KWANZA:LUGHA
## Muda: Saa 1 Dakika 40.

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**
**SOMA MAAGIZO YAFUATAYO KWA MAKINI .**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu, andika katika kijitabu hiki.
3. Ukiisha kuchagua jibu lako, lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala **sio** katika kijitabu cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU.**

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba umeandika yafuatayo katika karatasi ya majibu:

**NAMBARI YAKO YA MTIHANI**
**JINA LAKO**
**JINA LA SHULE YAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani nambari ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu, na usiikunje.
9. Kwa kila swali **1-50**, umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi **A, B, C, D**. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano**

**Katika kijitabu cha maswali:**

**Kutoka swali la 18 - 21, chagua jibu sahihi.**

**21.** Nomino 'nywele' ipo katika ngeli gani?

A. I - ZI
B. LI - YA
C. U - ZI
D. A - WA

Jibu sahihi ni **C**

Katika karatasi ya majibu

**18.** [A] [B] [C] [D]  **19.** [A] [B] [C] [D]  **20.** [A] [B] [C] [D]  **21.** [A] [B] [C] [D]

**21,** kisanduku chenye herufi **C** ndicho kilichochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku **kimoja** tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 8 zilizopigwa chapa.**

*Huchapishwa na kuratibiwa na taasisi ya uchapishaji ya Targeter Educational Publishers Ltd.*
*Email: info@targeterpublishers.co.ke*

**GEUZA UKURASA**

*Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.*

Baadhi ya Wakenya___1___tamaduni zao___2___hawajivunii kuwa wakenya. Hawajui maana ya uzalendo;___3___. Mtoto___4___anapokua ni muhimu alelewe mazingira yakuzayo tamaduni nzuri. Huenda akapata ufahamu zaidi hata kuliko___5___umri kwani___6___. Mila na tamaduni ni___7___maswala nyeti yanayofaa kuzingatiwa na kila mlezi.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | **A.** hushuhudia | **B.** hawahusudu | **C.** uhusudu | **D.** uhusudiwa |
| **2.** | **A.** ila | **B.** bali | **C.** na | **D.** wala |
| **3.** | **A.** hali ya mtu kuwa tayari kuifia nchi yake | **B.** hali ya mtu kutoipenda nchi yake | | |
| | **C.** hali ya kutoa msaada kwa wanaouhitaji | **D.** kuwahurumia na kuwasaidia wenzetu | | |
| **4.** | **A.** yoyote | **B.** wowote | **C.** yeyote | **D.** chochote |
| **5.** | **A.** wanamzidi | **B.** wanaomzidi | **C.** wanaomzidishi | **D.** wangezidi |
| **6.** | **A.** bahati hutaka ujasiri | **B.** mwacha mila ni mtumwa | | |
| | **C.** mwana mtamba kule hupita wazee wa kale | **D.** kila mja ana ujawe | | |
| **7.** | **A.** miongoni mwa | **B.** baadhi ya | **C.** katika | **D.** mithili ya |

Matatizo aliyokuwa___8___pendo___9___kuanza___10___lugha ya Kiswahili. Alijikakamua kadiri___11___. Baadaye___12___kushirikiana na wenzake ili afanikiwe. Silabi zilizo na sauti mbili kama vile___13___hazikumkanganya. Aidha alijifunza kuwa maneno kama vile wema, amani na upendo ni ___14___, sauti ghuna hazikuwa ngumu tena mifano ni___15___. Kwa kweli juhudi zake zilizaa matunda.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **8.** | **A.** nao | **B.** nayo | **C.** naye | **D.** navyo |
| **9.** | **A.** ndio ilifanya | **B.** ndilo lililofanya | **C.** ndiyo yaliyofanya | **D.** ndipo yaliofanya |
| **10.** | **A.** kukithamini | **B.** kuidhamini | **C.** kukidhamini | **D.** kuithamini |
| **11.** | **A.** alivyoweza | **B.** aliweza | **C.** aliyoweza | **D.** anaweza |
| **12.** | **A.** alikata kalima | **B.** alikata shauri | **C.** alikata kauli | **D.** alikata mate |
| **13.** | **A.** ndi | **B.** a | **C.** ng'a | **D.** ndwa |
| **14.** | **A.** nomino jumuishi | **B.** nomino za jamii | **C.** nomino dhahania | **D.** nomino za pekee |
| **15.** | **A.** ny, j, d | **B.** r, s, t | **C.** th, g, b | **D.** ny, h, f |

*Kutoka swali la 16 mpaka 30, chagua jibu sahihi.*

**16.** Maneno yafuatayo yanafuatana vipi katika kamusi?

*(i) Mshumaa*

*(ii) Mshawasha*

*(iii) Mufti*

*(iv) Mtomoko*

A. i, ii, iv, iii

B. iv, iii, ii, i

C. ii, i, iv, iii

D. ii, iii, i, iv

**17.** Bainisha aina za maneno katika sentensi ifuatayo

*Wachezaji wetu ni bora kuliko wao.*

A. Nomino, kivumishi, kitenzi, kivumishi, kihusishi, kiwakilishi.

B. Nomino, kiwakilishi, kitenzi, kihusishi, kiunganishi, kivumishi.

C. Nomino, kitenzi, kiwakilishi, kivumishi, kihusishi, kivumishi.

D. Nomino, kielezi, kitenzi, kihusishi, kiunganishi, kivumishi.

**18.** Akisami $\frac{5}{6}$ kwa maneno ni

A. tusui sita.

B. tusui tano.

C. humusi sita.

D. sudusi tano.

**19.** Ikiwa Jumapili ilikuwa mtondo, juzi itakuwa siku gani?

A. Ijumaa.

B. Jumanne.

C. Jumatatu.

D. Jumamosi.

**20.** Chagua sentensi iliyo katika hali ya mazoea

A. Shangazi anakuja nyumbani.

B. Dawati halijatengenezwa na seremala.

C. Maria huenda kanisani.

D. Musa atasafiri mwaka ujao.

**21.** Ni sentensi gani iliyotumia kivumishi kiulizi?

A. Makabati haya yalitengenezewa wapi?

B. Hawa watacheza mpira lini?

C. Wageni watapikiwa nini?

D. Barabara ilikarabatiwa lini?

**22.** Chagua jibu lenye kitenzi kutokana na nomino

A. Uharibifu - haribu.

B. Angaza - angavu.

C. Kilimo - mkulima.

D. Tulia - tulivu.

**23.** Onyesha sentensi iliyounganisha sentensi zifuatazo ipasavyo

*Mchezaji aliingia uwanjani kucheza*

*Mchezaji aliifungia timu yake bao*

A. Lau mchezaji aliingia uwanjani kucheza aliifungia timu yake bao.

B. Mchezaji aliingia uwanjani kucheza lakini aliifungia timu yake bao.

C. Mchezaji aliingia uwanjani kucheza kwani aliifungia timu yake bao.

D. Mchezaji aliingia uwanjani kucheza na kuifungia timu yake bao.

**24.** Chagua usemi halisi wa sentensi ifuatayo:
*Mwalimu alituonya kuwa tungekaidi amri tungeona cha mtema kuni*

A. "Mtakaidi amri na kuona cha mtema kuni", mwalimu alituonya.
B. "Msikaidi amri kwani mtaona cha mtema kuni", mwalimu alituonya.
C. "Mkikaidi amri mtaona cha mtema kuni", mwalimu alituonua.
D. "Mtakaidi amri mtaona cha mtema kuni", mwalimu alituonya.

**25.** Kinyume cha 'ziba' ni

A. fungua.
B. zibua.
C. usizibe.
D. zibia.

**26.** Nahau, *"hawapikiki katika chungu kimoja"*, huambiwa watu ambao hawasikilizani. *"kisebusebu na kiyoyo ki papo"*, huambiwa:

A. Mtu anayejifanya hataki kumbe anataka.
B. Mtu asiyetulia mahali pamoja.
C. Mtu mtukutu.
D. Mtu anayefanya mpango wa siri wenye nia mbaya.

**27.** Chagua umoja wa, *"makabati haya yao yalitengenezwa na maseremala wale."*

A. Kabati hilo lao lilitengenezwa na seremala yule.
B. Kabati hizi zao zilitengenezwa na seremala wale.
C. Kabati hili lao ilitengenezwa na seremala yule.
D. Kabati hili lao lilitengenezwa na seremala yule.

**28.** **Tegua kitendawili:**
*Mfalme hushuka kwa kelele.*

A. Samaki.
B. Kifo.
C. Mvua.
D. Nzi.

**29.** Bainisha matumizi ya **'ki'** katika sentensi
*Mvua ilikuwa ikinyesha tulipowasili shuleni.*

A. Kuonyesha masharti.
B. Kuonyesha hali.
C. Kuonyesha ngeli.
D. Kuonyesha kielezi.

**30.** Chagua sentensi iliyoakifishwa ipasavyo

A. Ajenda zote -zile zilizojadiliwa mkutanoni -zilifaa.
B. Shule hizo zilifungwa!tutajiunga na nyingine.
C. Mbunge (aliyechaguliwa) eneo bunge letu ni (mwenye) ujuzi.
D. Lahaula, joka hilo refu, utaliua?

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 mpaka* ***40.***

Elimu ni mojawapo ya mahitaji ya kimsingi katika maisha yetu. Taifa lisilowahakikishia wananchi wake elimu bora hujidunisha; hali hii si tofauti na kunguru mwoga anayekimbiza mbawa zake huku akiwaacha vifaranga wake kufa kwa njaa.

Malengo ya elimu shuleni ni yap? Kwa nini tunajizatiti kupata elimu? Yamkini tunatumia muda na rasilimali nyingi darasani ili kupata maarifa ambayo jamii itagharimia baadaye. Jambo hili litatuwezesha kujipatia riziki na hatimaye kuimarisha maisha yetu. Ingawa ni ukweli ulio wazi kuwa elimu hutupatia mbinu na maarifa yanayotuwezesha kuuweka mlo mezani, kuna manufaa mengi yanayotokana na elimu.

Elimu hukufanya kiumbe kamilifu kwa njia nyingi. Hupanua uwezo wako wa kuelewa mambo mbalimbali yanayoathiri maisha yako. Miongoni mwa mambo haya ni afya, uchumi na masuala ya kisiasa. Aliyeelimika ana uwezo wa kipekee wa kupata habari jinsi ya kuishi kwa siha njema. Aidha aliyeelimika ana uwezo wa kufanya maamuzi ***tasawari*** kuhusiana na uchumi na siasa hususan kutokana na mbinu anuwai za kupata habari na uwezo wa kuzitathmini.

Uwezo wako wa kuwazia mambo hupigwa msasa kupitia elimu. Kinyume na siku za kisogoni, kupata habari kumerahisishwa na ukuaji wa teknolojia mathalan mtandao wa kijamii. Changamoto iliopo ni jinsi ya kupata habari ya kweli na kubaini uvumi, habari iliyo muhimu na masihara; iliyokamilika na isiyo kamilifu. Bongo lililoelimika lina uwezo wa kuziweka habari kwenye mizani na kukata shauri ni zipi zinazofaa.

Jamii hunufaika na watu walioelimika. Jamii itakuwa katika hali gani bila ya madaktari, walimu, wahandisi, madereva au mawakili? Watu wenye taaluma tofauti tofauti hutekeleza majukumu yao katika jamii na kuifanya mahali pazuri pa kuishi. Ama kwa yakini, uvumbuzi uliowahi kufanywa kuimarisha jamii kwa asilimia kubwa umefanywa na mabongo ya watu walioelimika. Kwa kweli mtu aliyeelimika aghalabu hufikiria namna ya kuimarisha jamii kwa kuwasilisha mbinu mbadala na zifaazo za kufanya mambo.

Utangamano je? Tunapoelimika tunapata ufahamu zaidi kuhusu watu tofauti tofauti; utamaduni wao, mila na desturi zao na kuwakumbatia kama sehemu ya jamii pana. Kwa njia hii vurugu zisizofaa huepukika. Ushirikiano wetu huimarika ili kutimiza malengo yaliyo mazuri kwetu sote. Ni dhahiri kuwa kuna mengi yanayotokana na elimu. Sio ajabu kuwa serikali na familia zetu hutenga kiasi kikubwa cha pato kununua vitabu na vifaa vingine vya elimu, mishahara ya walimu na kukuza miundombinu. Yafaa sote tuelewe kuwa elimu ni bahari.

31. Kulingana na aya ya kwanza
A. taifa lisiloelimisha wananchi wake hupoteza heshima yake.
B. wananchi wasioelimika vizuri huathirika anapoachwa na mlezi.
C. taifa lenye ubinafsi huhatarisha maisha take.
D. mtu mwoga hushindwa kuwajibikia wanawe kama mlezi.

32. Kwa mujibu wa aya ya pili elimu
A. huimarisha hali ya maisha.
B. hutupatia riziki yetu ya kila siku.
C. hutusaidia kupata manufaa mengi maishani.
D. hutupatia ujuzi na maarifa ya kuishi maisha mazuri.

33. Elimu humsaidia mtu kuishi kwa siha njema namna gani?
A. Kuna habari za kutosha kuhusiana na siha njema.
B. Humwezesha mtu kuchunguza habari kwa makini zaidi.
C. Humwezesha mtu kupata pesa za kugharamia matibabu.
D. Mtu anaweza kutofautisha habari muhimu na masihara.

34. Watu waliopata elimu bora
A. hujitegemea.
B. huwa na afya nzuri kuliko wenzake.
C. huelewa mambo kwa mapana.
D. hufanya maamuzi bora zaidi.

35. Katika jamii, watu walioelimika
A. hupata faida tele kutokana na jamii.
B. hufanya uvumbuzi kutokana na mabongo yao.
C. hubuni mbinu mbadala za kuimarisha jamii.
D. hufanya kazi bora na hutekeleza majukumu yao kwa ufasaha.

36. Kulingana na kifungu utangamano hupatikana kwa njia gani?
A. Kwa kuwaelewa na kuwakubali wenzetu.
B. Kwa kuepuka vurugu zisizofaa.
C. Kupitia utimizaji wa malengo yetu.
D. Kwa kushirikiana pamoja.

37. Chagua maelezo yanayodhihirisha maana ya methali, *"Elimu ni bahari."*
A. Ni muhimu kila mtu kuwa na elimu.
B. Elimu huwezesha mambo yasiyoeleweka yakaeleweka.
C. Elimu ya mtu haiwezi kuibika.
D. Elimu haiishi na ni vizuri kuendelea kujifunza.

38. Mwandishi amedhihirisha kwamba elimu:
A. hutoshelesha mahitaji yetu.
B. ni ufunguo wa maisha bora.
C. hutuwezesha kupata habari.
D. huzuia migawanyiko katika jamii.

39. Chagua maana ya ***tasawari*** kwa mujibu wa kifungu.
A. Vutia.
B. Eleweka.
C. Pendeza.
D. Isiyofaa.

40. Mawazo makuu katika kifungu hiki ni
A. Elimu na manufaa yake kwa jamii.
B. Elimu na jamii iliyostaarabika.
C. Elimu na maisha bora kwa wananchi.
D. Vitabu na walimu shuleni.

*__Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 mpaka 50.__*

Simba aliishi katika msitu mmoja mkubwa sana. Simba huyo alikuwa mfalme wa wanyama wote porini. Alilitawala pori hilo hivi kwamba wanyama wote walimpenda na kumtii. Kila mwanzo wa mwaka, wanyama wote walijumuika kwake ili kumlipa pango. Wengine walitoka mapangoni, chini ya mawe, miti, viota na kwenye milima na mabonde. Walisimama gwarideni na mfalme angeamua kodi ambayo kila mmoja angelipa. Gharama hiyo haikuwa ghali na simba alihakikisha kuwa ni ile ambayo kila mmoja angeimudu. Malalamiko yalikuwa muhali kuzuka ila mamba ndiye aliyekuwa akileta ghadhabu zake kila wakati. ***__Tabia hii ya mamba iligeuka kuwa kia cha mwili__***.

Mwaka mpya ulipoanza, wanyama wote waliwasili nyumbani kwa simba kulipa kodi. Kama ilivyokuwa kawaida, mamba hakuwa miongoni mwao. Wakati huu tabia ya mamba ilikuwa imemfika mfalme kooni. Hakuwa tayari kupokea vijisababu vyake na alisisitiza kuwa lazima mamba alipe shilingi kumi kwa kuishi majini. Lakini maadamu simba alikuwa karimu, alimruhusu kulipa hela hizo kabla ya mwaka kukamilika. Mamba mwishowe alifika lakini aliondoka kwa mfalme kwa manunguniko. Mnyama wa mwisho kufika kwa mfalme alikuwa nyani mkondefu aliyeruhusiwa na mfalme kulipa senti kumi kwa kuishi kwa mti mrefu kuliko yote. Nyani alilipa senti hizo na kushika njia kuelekea makao yake.

Alipofika mwisho wa njia karibu na mnazi kwenye mto, nywele zilimsimama, ***__woga mkubwa ukamtawala__*** kwa woga akauliza, "kuna yeyote hapa?" hakutarajia jibu la swali hili. Kwa kuwa giza lilikuwa limeanza kubisha hodi, alijaribu kuyakodoa macho yake ili aone. Kwa mshangao macho yake yalikutana ana kwa ana na macho mawili mekundu.

"Ni mimi rafiki yako mamba. Nimekuwa nikikungoja hapa ili nikuvushe mto huu. Nina jambo zuri la kukuambia. Ubongo wa nyani ukazubaa na kabla ya kurejelea fahamu zake, tayari alikuwa mgongoni pa mamba akielea juu ya maji. Walipofika katikati ya mto, mamba akaanza kuzama. Sehemu tu iliyobaki kwa nyani ni kichwa cha mamba alikokalia karibu na mdomo wake. Hapo ndipo mamba alipomwambia nyani alipe nauli ya shilingi kumi. Alifahamu wazi kuwa nyani hangeweza gharama hiyo. Nyani alimwambia kuwa alikuwa tayari amelipa kodi yake ya senti kumi. Nyani alijikuta mashakani, mamba alimtishia kumla iwapo hangemlipa.

Wazo likamjia nyani akafurahi sana. Akakumbuka jinsi mamba wanavyopenda nyama ya figo. "Acha aibu ndogo ndogo! wewe wajua nyani kweli?" wakati mamba alipouliza alichomaanisha, Nyani alimwambia kuwa siku hiyo Jumatatu ni siku ambayo nyani huosha figo zake na alikuwa ameziosha ili kukaushwa na jua. Akamwarifu kuwa tayari alikuwa karibu kuupanda mti ili aziagize kabla ya kukutana naye. Alimweleza kwa ufasaha kuwa angemrejesha kwenye mnazi wake, angepata figo za kula.

Ingawa mamba alikuwa mkubwa kwa kimo, akili zake zilikuwa ndogo. Alipowazia figo zilizooshwa na kukaushwa kwa jua tamaa yake iliongezeka maradufu. Akasalimu amri na kumrejesha nyani alikomtoa. Baada ya kuupanda mti, nyani alimwambia mamba afungue mdomo ili azipokee figo zake. Nazi ilitua kwenye kinywa cha mamba. Mamba akalia kwa hasira na huzuni. Asubuhi iliyofuata, mamba hangeweza kumeza kitu chochote kutokana na uchungu mdomoni.

**41.** Kulingana na aya ya kwanza

A. mfalme alitawala himaya yake kwa hekima.

B. mfalme aliitaka tu kodi iliyolipwa na wanyama.

C. mfalme aliitawala himaya yake kiasi kuwa wanyama waliishi kwa umoja.

D. mfalme alipendwa na wanyama wote katika himaya yake.

**42.** ***"Tabia hii ya mamba iligeuka kuwa kia cha mwili"*** ina maana kuwa

A. ilikuwa tabia ya mamba kulalamika.

B. mamba alikuwa na hasira.

C. mamba alimdharau mfalme.

D. yalikuwa mazoea mamba kutolipa kodi kila mwaka.

**43.** Mamba alilipa kodi yake

A. mwanzoni mwa mwaka.

B. mwisho wa mwaka.

C. kwa kuwa mdaiwa mwaka mzima.

D. wakati wowote wa mwaka.

**44.** Kwa nini nyani alifurahi sana wazo lilipomjia akilini?

A. Aligundua kuwa mamba hawajui mengi kuhusu nyani.

B. Alijua alikuwa salama bila figo zake.

C. Alikumbuka jinsi mamba wanavyopenda nyama ya figo.

D. Aligundua njia ya kujiokoa.

**45.** Mamba alianza kuzama majini kwa kuwa alitaka

A. kumtia hofu nyani.

B. alipwe nauli na nyani.

C. kumla nyani.

D. nyani apige mbizi majini.

**46.** Akili za nyani zilizubaa kwa kuwa

A. aliogopa sana.

B. alifurahishwa na mamba.

C. alichanganyikiwa.

D. alikuwa kwenye shida.

**47.** Ni siku gani ya juma ambapo mamba hangeweza kumeza kitu chochote?

A. Jumatatu.

B. Jumanne.

C. Jumatano.

D. Jumapili.

**48.** Funzo hasa linalotokana na kisa hiki ni

A. tuwasamehe wenzetu.

B. tulipe kodi yetu inavyostahili.

C. tuvune tulichopanda.

D. tutumie akili zetu ipasavyo.

**49.** Ni dhahiri kwamba

A. nyani alikuwa mwerevu.

B. nyani alikuwa mwaminifu.

C. nyani alikuwa katili.

D. nyani hangeweza kuaminika.

**50.** Kauli, ***"woga mkubwa ukamtawala"*** imetumia tamathali gani ya usemi?

A. Sitiari.

B. Tashhisi.

C. Nahau.

D. Tashbihi.